



## Kilicho ndani ya Kasha



Kiunzi Bapa



Skrubu za Mashine aina ya M6 (4).



Skurubu aina ya M6 yenye Ncha Bapa (4)




Nati zenye Kifungo aina ya M6 (4)



Ufunguo wa Pembe Sita wa Milimita 4

## Zana Zinazopendekezwa



Keekee / Bisibisi ya Umeme




Msumari wa Keekee wa Milimita 6 (inchi 1/4)




Soketi Milimita 10




Spana malaya Milimita 10



## 1 | **Pakua Programu ya Starlink**

Changanua msimbo wa QR ili upakue Programu ya Starlink.






setup.starlink.com





## 2 | **Tafuta Eneo la Kufunga**

Starlink yako inahitaji mwonekano wazi wa anga ili iweze kuendelea kuunganishwa na setilaiti zinaposonga juu. Vitu vinavyozuia muunganisho kati ya Starlink yako na setilaiti vitasababisha ukatikaji wa huduma. Tumia zana ya vizuizi iliyo katika Programu yako ili kuhakikisha kwamba umechagua eneo linalofaa la kufunga.









### 3 | **Funga Kiunzi Kwenye Starlink**

Funga bolti za milimita 16 ulizopewa kupitia kiunzi ziingie kwenye sehemu ya nyuma ya Starlink. Funga bolti nne ukitumia ufunguo wa pembe sita kufunga Kiunzi Bapa mahali pake. Kaza skurubu kwenye kona zote 4 hadi bolti zifikie Nm 7 (lb-ft 5.2). Hakikisha kiunzi kimeunganishwa imara kwenye Starlink.



### 4 | **Tia Alama Matundu ya Kufunga**


Kwa kutumia Kiunzi Bapa kama mwongozo, weka alama kwenye matundu manne ya kufunga kwenye eneo la kufunga unalotaka kwa kutumia kalamu au penseli.

Skurubu za mashine zilizojumuishwa zinaweza kutumika kwenye sehemu za kufungia zenye unene wa hadi milimita 19 (3/4").

## 5 | **Toboa Matundu ya Kuelekeza**

Toboa mashimo kwa msumari wa keekee wa milimita 7 (inchi 9/32).


Lainisha mikwaruzo kwenye matundu hayo na uhakikishe kuwa sehemu hiyo haina vifusi.




## 6 | **Chomeka Kebo ya Starlink**

Fungamanisha ncha ya kiunganishi cha Performance ya kebo ya Starlink iliyoonyeshwa kwa mkato mwekundu na uichomeke kwenye Starlink yako kwa kushikilia ncha ya plagi na kuingiza kabisa kwenye sahani.

Ikiwa kebo ya Starlink inahitaji kuondolewa, zungusha kola kinyumenyume kisha uvute ili uitenganishe na Starlink yako.



### 7 | **Funga Skurubu**

Funga skurubu za mashine za milimita 4 35 ndani ya mashimo yaliyotobolewa mapema kwa kutumia ncha ya soketi ya milimita 10 na spana malaya. Kaza skurubu kwenye kona zote 4 hadi bolti zifikie Nm 8 (lb-ft 5.9).

